
Ujasiria mali
Njia na Namna ya Kufikia
MAFANIKIO YA KIFEDHA
...elewa Jinsi ya Kuwekeza Ondoa Umaskini
Na
Robert C.K

SURA I: UTANGULIZI

Mafanikio – waweza sema maendeleo ni jambo ambalo watu na mataifa yote duniani huhitaji zaidi ya kitu kingine. Ni hulka ya asili ya mwanadamu.

Mafanikio Kiteknolojia, Kiuchumi, Biashara, Elimu n.k ambayo pamoja na mambo mengine hupelekea kuboreka kwa maisha kwa kuongezeka kipato kutoka kipato duni kwenda kikubwa ndiyo haja ya kila mmoja wetu. Yote hayo huhitajika kama nyenzo muhimu katika kurahisisha maisha. Katika hili, mwana falsafa wa zamani Mohandas Gandhi anasema "**mafanikio hatua kwa hatua ni kanuni ya maisha, na mtu yeyote anayejaribu kwenda kinyume ili kulinda mtazamo wake hujikuta katika mwelekeo potofu"**. Naye Aristotle anasema "**mwanadamu ni mnyama mtafuta mafanikio. Maisha yake yana maana pale tu ambapo anainuka na kupambana ili kufikia malengo yake**". Hivyo suala la kutafuta mafanikio (kwa sasa ya kifedha) ni lazima, sharti na wajibu. Na usipofanya hivyo utaishia kuadhirika.

Yapo mafanikio ya aina mbalimbali na katika nyanja tofauti kama nilivyotaja chache hapo juu ambayo hupelekea maisha kuwa bora kuliko awali. Katika kitabu hiki tutazungumzia zaidi mafanikio ya kifedha katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na **biashara (ujasiria mali)**, **sanaa** na **michezo**. Pamoja na mambo mengine tutajikita zaidi katika kuangalia Njia na Namna za Kufikia Mafanikio hayo. Lengo kuu ni **kukufahamisha** *(inform)* juu ya mafanikio kwa ujumla, **kukuchochea** na **kukuonyesha** nini cha kufanya ili ufikie mafanikio ya kifedha.

Katika Sura hii ya kwanza tutaangalia kwa undani maana ya neno "**mafanikio**", aina za mafanikio na mifano ya watu waliofanikiwa katika maeneo mbalimbali. Pia tutaangalia falsafa ya mafanikio. Ambapo katika hili utabainishwa kuwa suala la kufanikiwa siyo la bahati au hatima *(fate and destiny)*. Yaani siyo kwamba mafanikio ni kwa ajili ya watu fulani tu kama dhana hiyo ilivyojengeka miongoni mwa wengi. Kila mtu anaweza kufanikiwa kwa kiwango atakacho. Siri ya mafanikio iko katika **mtazamo** *(mindset)*, **malengo**, **nia** na **juhudi** za mtu. Mtazamo chanya *(positive mindset)*, malengo maalum, nia dhabiti na juhudi binafsi ndivyo huamua mafanikio kati ya mtu na mtu hata taifa. Tatizo ni kwamba wengi hatuna maono na malengo. Kwamba tunataka kufanya nini maishani, hatuna hilo! Na wachache wenye malengo ama hawana nia dhabiti kuyatimiza au hawajui nini cha kufanya ili kufikia malengo yao. Zaidi ni kwamba uoga wa kuthubutu, kuto-jitambua na uvivu ni miongoni mwa mambo yanayotufanya na kutukwamisha tusifanikiwe.

Sura ya pili inaelezea kutambua tatizo na uhitaji. Ni lazima utambue tatizo kwanza ndipo ulikabili. Kwa mujibu wa mada yetu tatizo ni **ukosefu/upungufu wa fedha** za kutosheleza kumudu mahitaji yanayotukabili. Umaskini – wa kipatao ndiyo tatizo. Sura ya tatu inabeba ujumbe wa msingi wa kitabu yaani **"njia na namna za kufikia mafanikio ya kifedha"**. Katika sura ya nne tutaangalia kuhusu maono na jinsi ya kuweka malengo. Suala la kuweka malengo ambayo ndiyo huwa msingi wa utendaji ni la muhimu sana. Ndiyo mwongozo. Hakikisha unaweka malengo kwanza. Sura ya tano na ya mwisho ni juu ya

kuanza utekelezaji *(getting started)*. Hapa tutaangalia kwanza vizuizi *(barriers)* ambavyo vinawafanya wengi wasifanikiwe. Hii ni hatua muhimu katika kuendea utekelezaji. Baada ya hapo tutaangalia nini cha kuanza kufanya katika eneo ulilochagua katika kutafuta pesa. Na mwisho tutaangalia namna mbalimbali za kuweza kupata mtaji.

Kwa kuwa kuinua kipato na hatimaye kuondokana na umasikini ndiyo haja ya kila mmoja wetu, ni vyema basi kupata ufahamu huu juu ya njia na namna za kufikia mafanikio ya kifedha na kuzitendea kazi. Kwani bila hivyo utaendelea kubakia kama wengine tu wasio na uelewa kuhusu hili. Ninashauri usome kwa makini sura ya kwanza kwani ndiyo msingi wa kitabu hiki. Soma kidogo kidogo kila siku (sura moja kila siku siyo mbaya) hadi ukimalize ili uwe unapata muda wa kufikiri/kutafakari juu ya kile ulichokisoma. Usitake kusoma na kukimaliza kwa siku moja au masaa tu – kwani wengine tumejaliwa kusoma kwa spidi utadhani cherehani. Nakala hii siyo kama gazeti la habari za kawaida ulizo zowea, ni maisha yako mwenyewe.

1.1 MAFANIKIO NI NINI?

Katika maana ya jumla ya neno "mafanikio" Kamusi ya Kiswahili ya TUKI inasema ni hali ya **kufikia kile ulicholenga kukipata**. Kupata kitu ulichokiwekea malengo. Kwa mfano ukipanga kuwa na magari saba ndani ya miaka mitano na ukayapata kweli basi unahesabika kuwa umefanikiwa. Hivyo mafanikio yoyote katika eneo lolote huja kufuatia malengo yaliyowekwa. Ukipata kitu

chochote (gari, nyumba au fedha kwa mfano) bila kupanga usihesabu kama mafanikio kwako.

Na hiyo ndiyo maana ya jumla ya neno mafanikio, "**kufikia kitu/jambo ulilolenga**". Kwa mujibu wa mada yetu, mafanikio ninayozungumzia hapa ni yale ya kifedha *(financial success)*. Hali ya kufikia kuwa na kipato kikubwa cha kukuwezesha kumudu mahitaji yako na kuwa na ziada *(surplus)* kubwa. Kuwa na mapato yanayotokana na vitega uchumi na shughuli nyingine tofauti na ajira - ya ofisini tu.

1.2 AINA ZA MAFANIKIO

Kuna aina kuu tatu za mafanikio. Kumbuka kutofautisha kati ya *maeneo au nyanja za mafanikio* na *aina za mafanikio*.

Aina ya kwanza ni **mafanikio binafsi kifedha**. Au kwa kifupi "mafanikio ya kifedha". Ya pili ni **mafanikio mtambuka**. Haya ni zaidi ya kuwa na fedha. Na tatu ni **mafanikio kwa umma**. Tofauti na aina nyingine, mafanikio kwa umma hayahusishi wala kuhesabika kwa mhusika kuwa na fedha bali kile alichokifanya kwa ajili ya umma wake. Japo wengine hushindwa kutofauitisha kati ya aina ya pili na ya tatu na hivyo kuzichukulia kama moja, sisi tutaziangalia aina zote tatu.

Kila aina ya mafanikio ina faida/uzuri na ubaya au ugumu wake. Pia watu wenye kuyataka mafanikio fulani wana tabia na sifa maalum kama ifuatavyo:-

1.2.1 MAFANIKIO BINAFSI KIFEDHA – *Financial success*

Haya ni mafanikio ambayo mhusika husesabiwa kuwa nayo kwa kuangalia fedha au utajiri alionao. Kiasi cha **fedha** ndiyo kigezo kikuu. Mafanikio haya hupatikana kwa kufanya biashara au shughuli nyingine yoyote ile yenye kipato kikubwa mbali na ajira za maofisini. Kusudi la msingi la mhusika katika aina hii ya mafanikio kwa shughuli afanyayo ni kupata fedha/faida. Mafanikio haya yanajumuisha watu wanaojihusisha na vitu kama biashara, sanaa, michezo n.k.

Uchunguzi unaonyesha kwamba mhusika hunufaika kwa asilimia kubwa (kama 80%) na jamii asilimia ishirini (20%).

Mgawanyo/uwiano wa unufaikaji
- Mhusika = 80%
- Jamii = 20% (kupitia ajira, bidhaa, huduma n.k)

1.2.1.1 Faida/uzuri wa mafanikio ya kifedha

i. Humuwezesha mhusika kumudu gharama za maisha ya kila siku
ii. Mhusika hunufaika zaidi na kile anachokitabikia/kipata
iii. Mara nyingi ni kichocheo cha aina nyingine za mafanikio
iv. Ni rahisi kuyapata kuliko mafanikio aina nyingine

1.2.1.2 Ubaya/mapungufu yake

i. Hayana faida sana kwa umma
ii. Yanaweza kumpoteza mhusika asipoyatumia vizuri
iii. Hayana utukufu sana kama aina ya pili na ya tatu

1.2.1.3 Tabia na nia za watu wenye kuyataka mafanikio haya

i. Nafsi zao ziko juu katika kutaka mafanikio ya kimwili
ii. Hawapendi kuwa chini ya mtu, tegemezi au ombaomba
iii. Hali ya uzalendo wao ni ya kawaida tu, iko chini. Hujifikiria wao wenyewe zaidi kuliko nchi/umma
iv. Ni wachapa kazi kwa ujumla

1.2.1.4 Nyanja (maeneo) ya mafanikio ya kifedha

i. Biashara
ii. Michezo
iii. Sanaa
iv. Uvumbuzi wa kisayansi na teknolojia na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano (mtandao)

1.2.1.5 Mifano ya watu maarufu waliofanikiwa kifedha

JINA	ENEO/ NYANJA	SHUGHULI	KIPATO KWA WIKI (Tsh) - 2011	NCHI/ MAHALI
Reginald Mengi	Biashara	Vyombo vya habari na viwanda	-	Tanzania
Bill Gates	Biashara	Teknolojia ya kompyuta	-	Marekani
Ophrah Winfred	Biashara na Sanaa	-	Bil. 9.14	Marekani
Bakhresa	Biashara	Viwanda	-	Tanzania
Pele (Edison Arantes do Nascimento)	Michezo	Mpira wa miguu *(Football)*		Brazil
Kobe Bryant	Michezo	Mpira wa kikapu *(Basketbal)*	Bil. 2.02	Marekani
Muhamed Ali	Michezo	Masumbwi	-	
Tiger Woods	Michezo	Gofu	Bil. 2.15	Marekani
Filbert Bayi	Michezo	Riadha	-	Tanzania
Michael Jackson	Sanaa	Muziki	-	Marekani
Remmy Ongala	Sanaa	Muziki	-	Tanzania
Judith Wambula (Lady JD)	Sanaa	Muziki	-	Tanzania
Stevin Kanumba	Sanaa	Uigizaji filamu	-	Tanzania
Mr. Bean	Sanaa	Uigizaji vichekesho	-	Uingereza
Mark Zuckerberg	Uvumbuzi matumzi/ mawasiliano ya mtandao	Matumizi ya mtandao (facebook)	Bil. 6.58	Marekani

1.2.2 MAFANIKIO MTAMBUKA – *Intermediary success.*

Hii ni aina ya mafanikio ambayo mhusika husesabiwa kuwa nayo si tu kwa kuangalia kiasi cha fedha alichonacho bali pia manufaa/mchango wa shughuli yake kwa ustawi/maendeleo ya jamii. Yaani mtu kuwa na fedha bila kujihusisha moja kwa moja na mambo ya kibiashara, sanaa, michezo n.k bali na vitu kama dini, siasa za kawaida, NGOs n.k. Fedha siyo kigezo pekee lakini ni kigezo muhimu katika mafanikio haya.

Ni mafanikio ambayo mhusika huyapata kwa manufaa yake na jamii pia. Lengo lake siyo kunufaika yeye tu bali na jamii yake pia – kiimani, kielimu, kiuchumi, kitamaduni na kimaendeleo kwa ujumla. Jamii hunufaika kwa takribani kiwango sawa na yeye mwenyewe. Waweza sema asilimia hamsini kwa hamsini.

Mgawanyo/uwianao wa unufaikaji
- Mhusika = 50%
- Jamii = 50%

1.2.2.1 Faida/uzuri wa mafanikio haya

i. Humnufaisha mhusika na jamii pia
ii. Yana utukufu zaidi ya mafanikio binafsi kifedha
iii. Ni rahisi kuyapata ukilinganisha na mafanikio kwa umma

1.2.2.2 Ubaya/mapungufu

i. Ni magumu kuyapata zaidi ya yale ya aina ya kwanza
ii. Wakati mwingine mhusika hunufaika kidogo kuliko jamii yake

1.2.2.3 Tabia na nia za watu wenye kuyataka mafanikio haya

i. Pamoja na kutaka fedha, nafsi zao ziko juu katika kutaka mafanikio juu ya mambo ya kiimani na kielimu dunia.
ii. Wanapenda zaidi kusaidia watu wengine (jamii)
iii. Hali yao ya uzalendo iko juu zaidi ya wale wa kundi la kwanza
iv. Ni wachapa kazi

1.2.2.4 Nyanja (maeneo) ya mafanikio haya

i. Dini
ii. Taaluma (elimu dunia katika uvumbuzi)
iii. Siasa za kawaida (Siyo za harakati za ukombozi)
iv. Mashirika yasiyo ya kiserikali na kifaida (NGOs)

1.2.2.5 Mifano ya watu maarufu waliofanikiwa katika kundi hili

JINA	ENEO/ NYANJA	SHUGHULI/MCHANGO KWA JAMII	NCHI/ MAHALI
Desmond Tutu	Dini	- Shughuli za kidini - Kutetea haki za kibinadamu- kupinga ubaguzi wa rangi. - Kuongoza kampeni dhidi ya mapambano maambukizi ya VVU	Afrika Kusini
Dalai Lama wa 14 (Tenzing Gyatso)	Dini	- Shughuli za kidini - Kusimamia na kuendeleza misingi ya kimaadili na mwenendo bora kwa Watibet	Tibet
Albert Einstein	Sayansi (elimu dunia)	Uvumbuzi kanuni za kisayansi	Ujerumani
Socrates	Elimu ya Filosofia	Kufundisha na kuendeleza Filosofia	Ugiriki
Vernon Fenandesi	Dini	Shughuli za kidini	Tanzania
Benny Hinny	Dini	Kuhubiri Injili	Marekani

1.2.3 MAFANIKIO KWA UMMA – *Public success*

Kama ilivyo katika mafanikio mtambuka, haya ni mafanikio ayapatayo mtu bila kujihusisha na mambo ya kibiashara. Tofauti na aina nyingine za mafanikio, mafanikio haya hayapimwi kwa mtu kuwa na fedha kama kigezo bali kwa kuangalia kile alichokifanya kwa nchi yake na dunia kwa ujumla.

Mafanikio haya yanajumuisha watu wanaojihusisha na siasa za ukombozi (viongozi wa kisiasa wa kawaida hawahusiki hapa). Yanahusisha viongozi wa mapinduzi/mabadiliko chanya (siyo lazima wawe wanasiasa). Lengo la msingi kwa wahusika wa kundi hili huwa ni kuikomboa jamii dhidi ya – unyonyaji, umasikini, ukoloni, ubaguzi wa rangi n.k.

Mgawanyo/uwianao wa unufaikaji
- Mhusika = 20%
- Jamii = 80%

1.2.3.1 Faida/uzuri

i. Huinufaisha jamii zaidi kuliko mhusika
ii. Huleta mapinduzi/mabadiliko chanya
iii. Utukufu ni mkubwa kwa mhusika wa mafanikio haya kuliko aina nyingine zote. Hukumbukwa na kuenziwa vizazi na vizazi kwa mchango wake kwa umma.

1.2.3.2 Ugumu/ubaya wake

i. Mhusika hunufaika kidogo sana kuliko jamii yake
ii. Siyo rahisi kupatikana. Ni magumu kuliko aina zote. Unaweza hata kupoteza maisha – kuuwawa.

1.2.3.3 Tabia na nia za watu wenye kuyataka mafanikio haya

i. Nafsi zao ziko juu katika kutafuta mafananikio ya umma
ii. Hali ya uzalendo wao iko juu mno kuliko wengine. Wanaipenda nchi na umma zaidi ya kitu kingine maishani mwao
iii. Ni wachapa kazi
iv. Hawapendi kuwa chini ya manyanyaso/uonevu

1.2.3.4 Maeneo (nyanja) za mafanikio haya

i. Siasa za mapinduzi
ii. Harakati za ukombozi/mabadiliko chanya *(liberation movements)*. Hili linaweza pia kufanywa na viongozi/watu wa dini, vikundi mbalimabli au mtu binafsi (siyo lazima ziwe za kisiasa).

1.2.3.5 Mifano ya watu maarufu waliofanikiwa katika kundi hili

JINA	ENEO	SHUGHULI	NCHI/ MAHALI
Julius K. Nyerere	Siasa za mapinduzi/ ukombozi	- Kupigania uhuru - Mapambano dhidi ya umaskini	Tanzania
Nelson Mandela	Siasa za mapinduzi/ ukombozi	- Kupigania uhuru - Kupambana na ubaguzi wa rangi	Afrika Kusini
Kim Ili	Siasa za mapinduzi	Mapinduzi ya kiuchumi	Korea
Che Guavala	Harakati za kimapinduzi/ ukombozi	Mapinduzi ya kisiasa	Argentina
Martin Luther King, Jr	Harakati za ukombozi	Kupigania haki za biandamu – kupinga ubaguzi wa rangi	Marekani
Mao Zedong	Siasa za mapinduzi – ya Kiuchumi	Kuanzisha na kuongoza mapinduzi ya kiuchumi	China

Hizo ndizo aina za mafanikio. Vipi, umependa ipi? Haa!, hutaki zote?!!

Waweza kuwa na mafanikia aina zaidi ya moja. Mtu mwenye mafanikio ya kifedha kwa mfano anaweza pia kuwa mwenye mafanikio mtambuka - hata ya umma, japo siyo mara nyingi.

1.3 KWA NINI MAFANIKIO BINAFSI KIFEDHA?!!!

Kama msingi au kusudi kuu la kitabu hiki, sehemu kubwa iliyobakia itakuwa juu ya mafanikio binafsi kifedha na siyo mtambuka au umma. Lakini bado ukitaka kujua zaidi kuhusu aina hizo nyingine za mafanikio ambazo ni maalum kwa wale wenye mlengo wa kupigania/kutetea au kusaidia jamii waweza kuwasiliana nami. Vitabu vinavyozungumzia **uongozi** na **maendeleo** vitakusaidia. Zaidi zipo makala *(articles)* kadhaa zinazozungumzia mambo hayo kwa undani. Lakini kwa sasa hebu tujikite kwenye mambo ya fedha.

Unapozungumzia mafanikio binafsi kwa ujumla wake ni dhana pana kwani yapo ya aina nyingi na tofauti. Yapo mafanikio binafsi kielimu, kiimani, kifedha, kiafya n.k Lakini kwa nini **mafanikio binafsi kifedha?!** Unajua, kila atafutaye kitu ana sababu inayomsukuma kufanya hivyo. Mtu hatafuti tu kitu bila sababu. Ndipo unatakiwa kujiuliza sasa kuwa, kwa nini utafute pesa – mafanikio ya kifedha! Eti, wewe unafikiri ni kwa nini! Nadhani hili liko bayana wala halihitaji kujadili kwani hata mtoto mdogo pia kichaa anajua ulazima wa kuwa nazo.

Katika aina hii ya mafanikio, sababu kubwa inayomfanya mhusika kuyatafuta ni ili aweze **kuondokana na umaskini wa kipato**. Awe tajiri na hivyo **kuweza kumudu gharama za maisha** ya kila siku. Zaidi ya hayo ni kwamba mafanikio ya kifedha ni **chachu ya mafanikio aina nyingine** – ya pili na ya tatu. Aina hii ya mafanikio humuwezesha mhusika kumudu gharama zinazohitajika katika kufanikisha mafanikio aina hizo nyingine. Kwa mfano kama unataka kuanzisha huduma ya kidini au NGO, itakuwa rahisi kwako kufanya hivyo endapo utakuwa vizuri kifedha.

Ukweli ni kwamba pamoja na kuwa na mafanikio mengine binafsi - kielimu, kiimani n.k, bado **utahitaji tu pesa**. Fedha! Wapo watu wengi wenye fedha lakini hawana elimu, imani, vyeo... na bado tunawanyeyekea na kuwatukuza kama wafalme. Hivyo, sambamba na kuwa na mafanikio binafsi ya aina nyingine **usiache kutafuta fedha**. Ni lazima uwe nazo kama kweli unataka kuishi vizuri hapa mbele ya jua.

Jamani, tangu zamani hata kabla ya enzi za akina Musa masuala ya mafanikio ya kifedha na utajiri yalikuwepo. Tena ni mpango na makusudi ya Mwenyezi Mungu mwenyewe kwamba tuwe na utajiri wote. Fedha, dhahabu, mifugo na mali nyinginezo lakini tusimsahau Yeye. Kuna baadhi ya watu wa imani fulani fulani wakiwemo Wakristo na Waislam wanadai kwamba mafanikio ya kifedha hayafai wala hayatakiwi kwa waamini. Hii siyo kweli. Ukimsikia mtu anasema hivyo huyo kaingiliwa na roho chafu zidanganyazo. Ni Shetani! Mungu anachokataza na kuonya ni kufuata fedha na kutaka mali zaidi ya kumtaka yeye kwanza.

Lakini hajakataza watu kuwa na **fedha – utajiri**. Kama ni hivyo, mbona unatumia pesa wakati unasema ni dhambi kuzitafuta/kuwa nazo?! Si uzitupe basi?! Unatoa wapi fedha za zaka, sadaka na changizo nyingine kwa ajili ya kazi ya Mungu ambazo anaagiza tumtolee?!! Watu wengine bwana!

Hata Misaafu (vitabu vitakatifu vya Mungu) - Biblia na Kuruani vinazungumzia juu ya kuwa na utajiri kwamba ni jambo jema. Biblia inasema **...Yesu Kristo alifanyika maskini hapa duniani japo ni tajiri ili kwamba sisi tupate kuwa na utajiri kwa umaskini wake** [1.1]**. "...mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote..."** [1.2]**. Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye** [1.3]. Je, ni mapenzi ya Mungu kwamba waamini wake wawe maskini na hivyo kutawaliwa?

Kuruani nayo inasema **"mali na watoto ni mazuri ya ulimwengu..."** [1.4] Zaidi Mtume Muhamadi anaambiwa, **"Je, Mwenyezi Mungu hakukuta u yatima na akakuhifadhi ... akakufanya tajiri kutoka kwenye umaskini wako? Kwa hiyo usiwatendee vibaya yatima"** [1.5]**.**

Sasa kama Mungu mwenyewe anawapatia watu wake utajiri, kivipi na kwa nini tena iwe dhambi kuwa tajiri?! Wenzetu wazungu wanafahamika zaidi kama watu wakarimu, watoaji na wenye roho nzuri, unafikiri kwa nini wako hivyo? Kwa ufupi ni kwamba hawana cha ziada kutuzidi bali wao wameendelea – **wamefanikiwa kifedha**. Ni matajiri na hivyo wana ukarimu wote. Na Mungu wanae. We acha kuzitafuta. Wenzio tutazisaka

na kuzipata kisha tutakutumikisha kwazo. Utakuwa kibarua wetu. Na mwisho wa siku mbinguni tutakuwa wote. Wewe hapo, mimi hapa.

1.4 DHANA (FALSAFA) YA MAFANIKIO

Suala la kufanikiwa ni la kimaamuzi zaidi na siyo la bahati au hatma *(fate/destiny)*. Hakuna mtu fulani au jamii fulani iliyopangiwa kufanikiwa – kuwa tajiri na nyingine kuwa maskini. Hakuna! Watu wote tuna nafasi sawa katika kupata mafanikio. Watu wengi ninaozungumza nao kuhusu mafanikio wanashindwa kupata jibu la kwa nini wengine wamefanikiwa maishani na wengingine hapana. Bila shaka hata wewe umewahi kujiuliza hivyo.

Je, umewahi kuongea na watu waliofanikiwa – kifedha wakakwambia walifanyaje? Kwa taarifa yako ukiachilia waliopata mafanikio kwa kurithi, wengine wote ukiwasikiliza utashangaa. Wametokea kwenye maisha/familia duni usivyoweza kufikilia.., Lakini sasa ni matajiri. Utajiri unaamua tu wewe mwenyewe kuuanzisha. Kuna tajiri mmoja pale Bukoba mjini (jina nalihifadhi). Ana magari ya biashara na ya kutembelea kadhaa. Majumba, gesti, mitumbwi ya kuvulia na biashara nyinginezo. Kipato chake ni mamilioni kwa siku. Anasema alianza kwa kuuza (kurusha) sigara na bigijii mitaani na kwenye mabaa akiwa na umri wa miaka kumi na nne enzi hizo (miaka ya sabini). Alitokea kijijini ambako wazazi wake na jamii yake kwa ujumla pale kijijini walikuwa maskini mno. Aliamua kukimblilia mjini kwa lengo la kutafuta maisha-pesa na hatimae

aweze kuikwamua familia yake. **Alikuwa na malengo**. Mawazo hayo kwamba akienda mjini atafanikiwa aliyapata wapi katika umri mdogo kiasi kile kwa kweli mimi sijui, sikuweza kumuuliza hilo.

Hakubahatika kusoma zaidi ya kuishia darasa la nne. Anaeleza kuwa kwa kukumbuka na kuzingatia hali ya kijijini aliyoiacha, alilazimika kujituma kwa bidii na nia akijua hana msaada mwingine zaidi ya kutafuta pesa yeye mwenyewe. Anasema baada ya miaka mitatu, tayari akawa amefungua kibanda akiuza bidhaa mbalimbali kama – sabuni, chumvi, mafuta, nk. Aliendelea hivyo ambapo hadi kufikia leo hii ni kati ya matajiri wakubwa mkoa wa Kagera.

Naye Warren Baffett (bilionea wa tatu wa dunia kwa sasa, 2011) anaeleza kuwa alianza kwa kuuza bigijii kama huyo tajiri wa Kagera akiwa na miaka nane tu. Lakini sasa ni bilionea. Jamani, utajiri uko ndani ya mtu mwenyewe. Amua, panga na chukua hatua ya utekelezaji... Hivi, kwa historia za maisha ya awali kwa hao jamaa ungetegemea watakuja kuwa matajiri?

Nimeweka tu mifano hiyo ya matajiri waliofanikiwa katika biashara. Lakini kama tulivyokwisha kuona, mafanikio ya kifedha si katika biashara tu. Wapo waliofanikiwa katika michezo kama akina Filbert Bayi, Muhamedi Ali na wengineo. Ukiwauliza ilikuwa kuwaje mpaka wakafikia mafanikio hayo utaona kuwa hawakufanikiwa tu kibahati nasibu. **Waliamua**. **Wakapanga**. **Wakatekeleza** na hatimae **KUFANIKIWA**!

Nadhani kwa maelezo hayo machache umenielewa kuwa mafanikio ni kuamua na kupanga. Kinacho takiwa ni kuwa na **sababu**, **nia, malengo** na **ari/shauku** *(**enthusiasm**)* ya mafanikio. Kwani ukiyakosa hayo ni sawa na gari kukosa kichapuzi *(accelerator)*. Unakosa msukumo.. nguvu ya kukupush mbele. Huwezi enda mahali eti!

Hizi hapa ni baadhi ya falsafa za msingi kuhusu kufikia mafanikio:

i. Mafanikio ni kwa ajili ya mtu yeyote. Ni suala la kuamua na kupanga/kuchagua

ii. Mafanikio ni mchakato na hatua. Siyo suala la kufikiwa kwa usiku mmoja tu

iii. Sababu, malengo, shauku (*enthusiasm*), nia na juhudi binafsi ndiyo mihimili ya kufikia mafanikio.

iv. Mafanikio yako katika kushinda hofu na upinzani wa kuto-kuthubutu. Ni wale tu wenye kuweza kuthubutu/kujaribu ndio watakao fanikiwa daima.

v. Mafanikio ni matokea ya kufanya kazi kwa bidii. Kuwa katika utendaji *(action)* kwa muda mrefu bila kuacha.

vi. Mafanikio ni matokeo ya utekelezaji wa jambo/kitu ulichokibeba au tunga *(conceive)* kukifanya.., waweza sema **maono**. Hapo ndiyo mwanzo wa yote.

Katika kuelezea dhana na falsafa ya mafanikio, watu kadhaa maarufu duniani wamepata kunena yafuatavyo:-

"Tofauti kati ya mtu afanikiwaye na wengine siyo kukosa nguvu wala maarifa, bali ni kukosa **nia**"
Vincent T. Lombardi

"Moja kati ya makosa ya wengi na moja ya mawazo ya hatari zaidi ni kuwaza kwamba mafanikio ni kwa ajili ya watu fulani wenye akili nyingi, u-sangoma fulani au mambo mengine ambayo sisi hatunayo. Ukweli mafanikio kwa ujumla ni kung'ang'ana na kutoruhusu yaondoke"
Maltbie Davenport Babcock

"Ni mtu mwenye kuendelea kwa umakini **hatua kwa hatua** na nafsi yake kupanuka zaidi na zaidi... atakayefikia mafanikio ya kiwango cha juu"
Alexander Graham Bell

"**Shauku** kubwa juu ya kitu chochote huleta uhakika wa kufanikiwa kwa kuwa shauku ya matunda huonyesha mbinu za kuyafikia"
William Hazlitt

"Mafanikio yanategemea maandalizi ya awali, na pasipo maandalizi hayo kuna uwezekano wa kutofanikiwa"
Confucius

"Niliumbwa **kufanya kazi**. Kama wewe ni **mchapa kazi** kikweli kweli, utafanikiwa kikweli kweli "
Johann Sebastian Bach
"Uzoefu unaonyesha kwamba mafanikio ni matokeo ya **nia**, **kiu** na **bidii** zaidi kuliko uwezo. Mshindi ni yule anayejitoa yeye mwenyewe kwa kazi yake - mwili na nafsi"
Sir Thomas Fowell Buxton

"Ili ufanikiwe vizuri ni lazima ufeli kwanza ili utambue kitu gani usikifanye tena wakati mwingine"
Anthony D'Angelo

1.5 FURSA NA CHANGAMOTO KATIKA MAFANIKIO

Katika kila kutenda na kufanikisha jambo kuna fursa au myanya na changamoto. Mambo haya mawili ni ya kawaida katika utendaji. Wakati fursa yakiwa ni mambo yanayoweza kukusaidia kufanikisha jambo endapo utayatumia vilivyo, changamoto kwa upande wake ni yale mambo yanayoweza kukufanya usifanikishe jambo endapo hutayakabili vilivyo. Ni kinyume cha fursa. Kwa mfano kama fursa iliyopo ni upatikanaji wa mikopo kirahisi, changamoto yake inakuwa kinyume – yaani kukosekana kwa mikopo.

Kwa hiyo katika kuamua nini cha kufanya katika kuendea mafanikio yoyote yale mtu unapaswa kuangalia myanya na wakati huo huo kukabiliana na changamoto husika.

1.5.1 Fursa katika mafanikio ya kifedha

Fursa kama tulivyoona hapo juu ni jambo/kitu kinachoweza kupelekea au kuchangia kufanyika na hata kufanikiwa kwa jambo fulani. Katika kuamua kufanya shughuli ya kukupatia fedha unapaswa kuangalia kwa umakini fursa zilizopo.

Fursa zinazo ambatana na mambo ya kutafuta fedha ni pamoja na vitu kama vile **soko**, **ushindani mdogo**, **uwepo wa mtaji**, **mikopo** n.k.

Kama kunawatu wa kushangaa ni wale ambao bado ni maskini na wakati huohuo wamezungukwa na fursa kadhaa za kuweza kuwatoa kifedha. Asiyeweza kutambua wala kutumia fursa hatakuja kufanikiwa katika jambo lolote. Huwezi hata kidogo! Angalia maneno haya hapa chini kuhusu kutumia fursa katika mafanikio.

"Watu wenye mafanikio makubwa hawakuyapata kwa kuwa na vipaji fulani au bahati. Walizitumia fursa zilizokuwa mikononi mwao"
Bruce-Barton

"Siri ya mafanikio maishani ni kwa mtu kuwa tayari dhidi ya fursa inapokuja"
Benjamin Disraeli

1.5.2 Changamoto katika mafanikio ya kifedha

Changamoto ni jambo lolote linaloweza kukwamisha au kuleta ugumu katika kufikia mafanikio. Ni kinyume cha fursa. Zipo changamoto za ndani (*internal challenges*) na za nje (*external challenges*)

a. Changamoto za ndani

Haya ni mambo yanayoweza kumkwamisha mtu asifanikiwa kutokana na yeye mwenyewe jinsi alivyo. Ni mambo ya ndani ya mtu mwenyewe ambayo yanajumuisha vitu kama vile **mtazamo**, **uelewa**, **imani** na tabia za kimwenendo kwa ujumla. Zaidi uvivu, uoga, ujuaji *(arrogance/overconfidence)* bado ni changamoto za ndani ambazo mtu anapaswa kuzishinda ili afanikiwe. Hizi ni changamoto mbaya kuliko zile za nje.

b. Changamoto za nje

Chanagmoto hizi ni zile za kimazingira na hali ya kiutendaji kwa zaidi. Hujumuisha vitu kama sera na sheria mbaya, kukosekana kwa soko, kuwepo kwa ushindani mkubwa, kukosekana kwa mtaji n.k. Mtu mwenye kukumbana na mambo hayo hulazimika kwa namna moja au nyingine kuyashinda ili kufikia malengo. Vinginevyo utabakia pale pale.

Hata hivyo changamoto hizo zinapaswa kutumiwa kama kichocheo cha kukufanya ujibidishe na kufanya vizuri zaidi.

Zitumie kama daraja/ngazi ya kukupeleka mbele. Usikubali zikukatishe tamaa. Zenyewe zipo tu, elewa hivyo kisha songa mbele.

Hebu angalia, pamoja na upinzani aupatao winga *(striker)* toka kwa walinzi wa timu pinzani katika mchezo wa soka, haimfanyi aache kujaribu kupenya na kutafuta gori. Anazuiwa, anakatwa mabuti lakini yupo tu. Na mwisho wa siku anapata bao. Unafikiri winga hao wangeacha kushambulia eti kwa sababu kuna upinzani (changamoto) toka kwa walinzi wa timu pinzani kungekuwa na kufungana kwenye soka?! Sasa wewe unataka walinzi (changamoto) wasiwepo kwenye soka, utamu wa soka utatoka wapi?!

Kadhalika katika kutafuta pesa. Vikwazo ni lazima viwepo na vitaendelea kuwepo ili utamu wa kuzipata uendelee kuwepo. We angalia namna ya kupenya kwenye hizo changamoto kisha fanya mambo. Songa mbele!